UTEKELEZAJI



Wananchi wa Wilaya ya Kilwa waliojitokeza kufyeka mashamba ya bangi katika vijiji vinne vya wilaya hiyo. **Picha na Mpigapicha Wetu**

# Mtego wa gunia moja ulivyofichua mashamba ya ekari 3,117 za bangi

**Elizabeth Edward,** Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Ilianza kwa gunia moja la bangi lililokamatwa katika mitaa ya Manzese jijini Dar es Salaam, baadaye likawa kama nyayo zilizofuatwa kwa uangalifu, hadi kufikia mabonde ya Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi yalipokutwa mashamba makubwa ya bangi.

Uchunguzi huo uliowezesha kubainika kwa ekari 3,117 za bangi ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya mkoa huo ambapo vijiji vinne, vitongoji vinane vya wilaya ya Kilwa vilibainika kujihusisha na kilimo hicho haramu.

Akizungumza katika mahojiano na Mwananchi, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo alisema ugunduzi wa mashamba hayo uliwashtua kwa kuwa Lindi haikuwa miongoni mwa mikoa ambayo mamlaka ilikuwa imeitambua kama eneo lenye uzalishaji mkubwa wa bangi.

"Kilichotokea Kilwa kilitushtua sana. Hatukuwahi kutarajia Mkoa wa Lindi unaweza kuwa na bangi nyingi kiasi kile," alisema.

Alisema baada ya operesheni kubwa zilizofanyika katika mikoa iliyokuwa ikiongoza kwa uzalishaji wa bangi kama Morogoro, Arusha na Mara, waliona mabadiliko katika njia za usafirishaji wa bangi iliyokuwa ikiingia Dar es Salaam.

"Awali, sehemu kubwa ya bangi iliyokuwa ikiingia Dar es Salaam ilikuwa ikitoka katika mikoa hiyo na kusafirishwa kwa kutumia magari makubwa ya mizigo, lakini baada ya operesheni kuimarika, njia hiyo ilianza kupungua.

"Baada ya kufanya operesheni mikoa ya Morogoro, Arusha na Mara na kupunguza kwa kiwango kikubwa, tuliona bado bangi inaingia Dar es Salaam. Tukaanza kujiuliza inatoka wapi," alisema.

Alisema uchunguzi huo uliwapeleka kwenye njia ya kusini baada ya kukamatwa kwa mtu aliyekuwa akisafirisha gunia moja la bangi kwa gari binafsi kutoka kusini kwenda Dar es Salaam.

Kukamatwa kwa mtu huyo ilikuwa sehemu ya mnyororo baada ya kuwakamata wavutaji bangi eneo la Manzese, ambao walimtaja anayewauzia na alipokamatwa naye alimtaja anayemletea.

"Baada ya kumpata huyo mtu tukamwekea mtego siku mletaji siku alipokuja kuleta mzigo. Tulidhani anatoa Morogoro, lakini alipoulizwa vizuri akasema anatokea mikoa ya kusini, hapo ndipo tukaanza ufuatiliaji mwingine kujua ni wapi hasa inatoka bangi hiyo," alisema.

Uchunguzi uliendelea hadi walipofuatilia hadi Kilwa ambako walikuta mtu mmoja akiwa na magunia matano ya bangi nyumbani kwake.

"Tulipofika Kilwa kwenye eneo ambalo yule mtu alisema ananunua kweli tuliwakuta vijana, tulipowakamata na kuwahoji wakatupeleka wanapoichukua ambapo ni nyumbani kwa mtu na tulimkuta mwenyewe na magunia matano ya bangi nyumbani kwake.

"Tulipomuhoji na yeye akasema ananunua kutoka kwa vijana wanaolima mabondeni. Ndipo tulipoenda huko na kuyakuta mashamba makubwa ya bangi," alisema.

Alisema uchunguzi umeonyesha kilimo hicho kilianza takribani miaka miwili iliyopita baada ya baadhi ya watu kuona fursa ya soko la bangi lililokuwa limepungua katika maeneo mengine.

"Walilima mwaka wa kwanza wakaona hawajabainika, mwaka jana wakalima tena. Tulifika kabla hata haijakomaa, ndio maana tukaweza kuifyeka yote," alisema Lyimo.

Alisema walipobaini hali hiyo waliwaita viongozi wa vijiji na vitongoji na kuwaeleza madhara ya kuacha kilimo cha chakula na kuingia kwenye bangi.

"Walikuwa wanalima mihogo, karanga, mpunga na mazao mengine, lakini wakaacha na kuingia kwenye bangi. Tuliwaeleza kuwa mwisho wake umaskini utaongezeka, hali ya chakula itakuwa mbaya na hata uhalifu unaweza kuongezeka," alisema.



Shamba la bangi lililokutwa katika Wilaya ya Kilwa. **Picha na Mpigapicha Wetu**

## Mbegu zilivyoingia Kilwa

Katika uchunguzi wa DCEA, kilimo hicho hakikuwa tu uamuzi wa wananchi wa kawaida, bali kulikuwa na viashiria vya watu kutoka nje kuwashawishi baadhi ya wakazi kuingia katika biashara hiyo.

Kamishna huyo alisema baadhi ya vijana wa eneo hilo waliwasiliana na watu ambao waliwapa mbegu za bangi na kuwaahidi kununua mazao hayo kwa bei kubwa.

"Walikuja na kuwashawishi walime bangi kwenye maeneo yao kwa sababu kuna maeneo ya vificho, mabondeni na katikati ya milima. Waliwaambia wao watanunua hiyo bangi na kuisafirisha kwa njia ya bahari," alisema.

Alisema uchunguzi bado unaendelea ili kubaini kwa uhakika watu hao walikuwa wanatoka wapi, lakini taarifa za awali zinaonyesha huenda walikuwa na mtandao wa watu waliokuwa na nia ya kusafirisha bangi kwenda maeneo mengine.

Anaongeza kuwa mbegu hizo zilikuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha kiasi kikubwa cha bangi.

"Mbegu sado moja unaweza kuotesha eneo kubwa, hata zaidi ya ekari tano. Walipewa mbegu hizo, wakalima kidogo mwaka wa kwanza na kuuza. Walipoona wenzao wameuza, mwaka huu wakalima bonde zima," alisema Lyimo.

**Ekari 3, 117**

**Ukubwa wa mashamba ya bangi yaliyokamatwa na kufyekwa wilayani Kilwa katika Mkoa wa Lindi.**

## Wananchi wameelimishwa

Lyimo alisema kabla ya kuanza operesheni ya kuyafyeka mashamba hayo, DCEA ilianza kwa kutoa elimu kwa wananchi na viongozi wa maeneo hayo kuhusu madhara ya kilimo hicho.

"Bahati nzuri tulianza na elimu kwa wananchi tukawahamasisha. Kila siku tulikuwa tunapata wananchi 250 hadi 300 waliokuwa wanajitokeza," alisema.

Kwa mujibu wa Kamishna huyo, tofauti na operesheni nyingine ambazo mamlaka hutumia gharama kubwa kuangamiza mashamba ya bangi, safari ya Kilwa ilikuwa tofauti kwa kuwa wananchi wenyewe walijitokeza kuyafyeka.

"Safari hii bangi yote imefyekwa na wananchi wenyewe. Sisi hatukutumia gharama yoyote kufyeka hizo ekari 3117," alisema.

Alisema mkakati wa DCEA sasa ni kuendelea kufuatilia chanzo cha kila dawa ya kulevya inayokamatwa ili kufikia maeneo inakozalishwa.

"Tunaangalia hii bangi imetoka wapi, chanzo chake ni kipi. Tunafuatilia mnyororo wote hadi tunafika kule inakozalishwa," alisema.

Alisema operesheni za kudhibiti uzalishaji wa bangi zitaendelea nchini kote, huku akiwataka wananchi kuacha kilimo hicho kutokana na madhara yake na hatari ya kupata kifungo cha maisha, endapo watakamatwa wakizalisha dawa za kulevya.

"Kilimo cha bangi hakina faida yoyote kwa mwananchi. Kilwa wamepata hasara kubwa kwa sababu walilima, wakapalilia wakisubiri kuvuna lakini tukaenda na kuifyeka yote," alisema.

## Wasemavyo wananchi

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Nandete walioshiriki operesheni hiyo walisema kilimo cha bangi hakina manufaa kwa jamii na kimeendelea kuhatarisha mustakabali wa vijana.

Mkazi wa kijiji hicho, Veronica Mandai, alisema wakati mwingine watoto hujihusisha na kilimo hicho bila wazazi wao kufahamu, jambo lililowasukuma wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika zoezi la kuteketeza mashamba hayo.

"Nawaomba vijana na wanawake wawe mstari wa mbele kukataa na kutokomeza dawa za kulevya kwa sababu zina madhara makubwa kwa afya na maendeleo ya jamii. Vijana ndiyo nguvu kazi ya taifa na wakijiingiza katika matumizi au uzalishaji wa dawa za kulevya watapoteza fursa ya kulijenga taifa," alisema Veronica.

Naye mkazi mwingine wa kijiji hicho, Nassoro Mbonde, alisema jamii imeanza kutambua kuwa faida za muda mfupi zinazotokana na kilimo cha bangi haziwezi kulinganishwa na madhara yake kwa familia na kizazi kijacho.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kandawale, Mohamed Mpame, alisema baada ya operesheni hiyo viongozi wa kata kwa kushirikiana na vijiji na vitongoji wataimarisha doria na usimamizi wa maeneo yao ili kuhakikisha kilimo cha bangi hakirejei.

"Tutahakikisha tunafanya doria za mara kwa mara na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi waachane kabisa na kilimo cha bangi. Nawashauri watumie ardhi yao kulima mazao halali yenye tija kama korosho," alisema Mpame.

**"Walikuwa wanalima mihogo, karanga, mpunga na mazao mengine, lakini wakaacha na kuingia kwenye bangi. Tuliwaeleza kuwa mwisho wake umaskini utaongezeka, hali ya chakula itakuwa mbaya na hata uhalifu unaweza kuongezeka,"**

Aretas Lyimo

MCL "Epaper Copy"